BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

TAARIFA YA MAONESHO YA TANO (5) YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI KIUCHUMI

KAULI MBIU

"Mifuko na Programu za Uwezeshaji kwa Uchumi Imara na Endelevu".

MEI, 2022

1.0 UTANGULIZI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC) limeanzishwa kwa Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004 kama chombo cha juu Kitaifa cha kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Lengo la Sera hii ni kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga na kumiliki uchumi wa nchi yao.

Majukumu makuu ya Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004 ni kukuza na kusaidia shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania; kuwapa watanzania fursa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi; kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji; na kuhimiza watanzania kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi.

1.1 SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI, 2004

Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mwaka 2004 ili kutoa mwongozo wa kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki kikamilifu katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Kwa maana hiyo, Sera za Kisekta zinatakiwa kuhakikisha zinatoa kipaumbele pale inapobidi kwa watanzania ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina nguzo tisa ambazo zikitekelezwa kwa ukamilifu zitawezesha watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa nchi na lengo kubwa la Sera ni kuwawezesha watanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga na kumiliki uchumi wa nchi yao. Aidha, Nguzo hizo zimeainishwa katika Mchoro Na.1.

Mchoro Na.1: Nguzo za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

1.2 MITAJI

Mitaji ni miongoni mwa nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ya mwaka 2004 inayotoa maelekezo kwa Serikali na wadau wengine kuwasaidia na kuwawezeshaji wananchi ili waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kupitia nguzo hii, Serikali ilianzisha mifuko n programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha pamoja na huduma nyingine za uwezeshaji ili kuwafanya wananchi washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao.

Madhumuni mahsusi ya mifuko hii ni pamoja na kutatua changamoto zinazozuia wananchi kutoa mchango katika kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vikwazo vinavyosababisha benki kusita kutoa mikopo kama vile gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo, ukosefu wa utambulisho rasmi, kutokuwa na taarifa muhimu za waombaji mikopo, ukosefu wa dhamana, udhaifu unaowafanya wananchi wasikopesheke, ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, ukosefu wa mitaji ya kuchangia uanzishaji wa miradi nk.

Walengwa wakuu wa mifuko ni wananchi wote nchini Tanzania wanaofanya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya kilimo, mifugo, maliasili na utalii, afya, viwanda na biashara, Ujenzi, Maendeleo ya ardhi, mawasiliano na uchukuzi, nishati, na elimu.

Baraza la Uwezeshaji linaratibu Mifuko ya uwezeshaji kwa njia mbalimbali kama vile vikao ambavyo hufanyika mara mbili kwa mwaka, kupokea taarifa, kuichambua, kuandaa taarifa ya pamoja, kufanya utafiti, ufuatiliaji na tathmini juu ya mifuko hii na kutoa mapendekezo kwa mamlaka husika pamoja na kuitangaza kupitia vyombo mbalimbali.

1.3 MIFUKO INAYORATIBIWA NA BARAZA NA MATOKEO YA UTENDAJI

Kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 Mifuko hii kwa pamoja imefanikiwa kutoa huduma za uwezeshaji kwa wananchi wenye thamani ya Shilingi bilioni 903. Aidha, fedha hizi zimewanufaisha wananchi 5,932,668 wakiwemo wanawake 3,737,581 (63%) na wanaume 2,195,087 (37%). Aidha kupitia uwezeshaji huu, mikopo iliyotolewa kwa walemavu ilikuwa ni shilingi bilioni 81.27 na kuwafikia jumla ya walemavu 640,723 ambao sawa na asilimia 10.8 ya wanufaika wote.

Mifuko hii ya uwezeshaji kupitia Shilingi bilioni 903 zilizotolewa, umenufaisha sekta mbali mbali kama ifuatavyo:- Sekta ya Afya imewezeshwa shilingi bilioni 63.21 (7%), imewezeshwa Shilingi bilioni 108.36 (12%), Sekta ya Kilimo (mazao, ufugaji na uvuvi) imewezeshwa shilingi bilioni 279.93 (31%), Sekta ya Utalii imewezeshwa shilingi bilioni 90.30 (10%) , Sekta ya Viwanda na Biashara imewezeshwa shilingi bilioni 207.69 (23%), Sekta ya nishati imewezeshwa shilingi bilioni 54.18 (6%), Sekta ya nyinginezo kama miundombinu, ujenzi nk zimewezeshwa shilingi bilioni 27.09 (3%).

Aidha, mifuko hii imetengeneza jumla ya ajira 7,712,468 ambapo katika ajira hizo, ajira kwa wanawake zilikuwa 4,704,605 (61%) na ajira kwa wanaume ni 3,007,863 (39%).

Pamoja na kuwa mifuko hii inaendelea kufanya vizuri, lakini tafiti kadhaa zilionesha kuwa mifuko hii haifahamiki na walengwa waliokusudiwa hasa wanaoishi katika maeneo ya vijijini na wanufaika wake wanajirudia rudia. Hivyo kuna mapendekezo kutoka kwa wadau yalitolewa ili kuhakikisha mifuko hii inafahamika, na miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuandaa maonesho ambayo yatakuwa yanafanyika katika kila kanda na kila mwaka.

2.0 CHIMBUKO NA HISTORIA YA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Maonesho ya Mifuko ni utekelezaji wa kikao cha wakuu wa Taasisi za Mifuko kilichokaa tarehe 25 Mei, 2015 katika ukumbi wa Mikutano, Ofisi za Tume ya Mipango, moja wapo ya changamoto iliyowasilishwa na Wakuu wa Taasisi ilikuwa ni kutofahamika kwa Mifuko hii, na pendekezo lililotolewa ili kufanya mifuko hii ifahamike ni kuandaa maonesho yatakayohusisha Mifuko yote ya Uwezeshaji, Wajasiriamali walionufaika na mifuko pamoja na kuzialika taasisi nyingine za Serikali na binafsi zinazofanya kazi sambamba na wajasiriamali.

Maonesho ya kwanza yalifanyika tarehe 18 - 22 Aprili, 2017 katika Viwanja vya Mashujaa Mkoani Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Waziri Mkuu Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa. Katika siku ya ufunguzi huo, Mhe Waziri Mkuu alitoa maagizo kwa Baraza kuendelea kuratibu maonesho kila mwaka Kikanda.Kupitia maelekezo haya, Maonesho yaliendelea kufanyika kama ifuatavyo:-

NA.	MWAKA	TAREHE	VIWANJA	KANDA	MIKOA ILIYOHUSISHWA
1	2017	18 - 22 Aprili, 2017	Mashujaa	Dodoma (Kanda ya Kati)	Dodoma, Singida and Tabora
2	2018	19 – 23 Oktoba, 2018	Luanda Nzovye	Mbeya (Nyanda za Juu)	Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma and Songwe
3	2019	14 – 20 Oktoba, 2019	Bariadi	Simiyu (Kanda ya kuzunguka Ziwa Viktoria)	Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu and Shinyanga
4	2021	07 -13 Februari, 2021	Sheikh Amri Abeid	Arusha (Kanda ya Kaskazini)	Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga
5	2022	08-14 Mei, 2022	Jamhuri	Morogoro (Kanda ya Mashariki)	Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara

3.0 MAANDALIZI YA MAONESHO YA TANO NA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Katika maonesho haya, kulikuwa na kamati kuu mbili zilizohusika katika maandalizi, aidha, kamati ya kwanza ilikuwa ya kitaifa iliyohusisha wawakilishi kutoka katika taasisi za mifuko na kamati ya pili iliwa ya Mkoa wa Morogoro iliyohusisha wafanyakazi kutoka katika sekta binafsi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Ofisi ya Manispaa ya Morogoro. Aidha, kila kamati ilikuwa na hadidu rejea za kazi pamoja na mpango kazi. Kila kamati ilikuwa inafanya vikao vya ufuatiliaji wa majukumu wanayopeana na kamati zote mbili (Morogoro na Taifa) zilikuwa zikikutana ili kupeana mrejesho juu ya hatua iliyofikiwa katika maandalizi.

Kamati ya Taifa ilihusisha wawakilishi kutoka Taasisi za mifuko 13 kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

1. Bi Edista Njau – **Benki Kuu ya Tanzania (BOT)** 2. Bw. Michael J. Karaghe - **Wizara ya Maliasili na Utalii** 3. Bi. Atupokile Elia - **Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Walemavu)** 4. Dkt. Juma Makaranga - **Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania (TACT**) 5. Bw. Brian T. Samwel - **Ofisi ya Rais (TAMISEMI)** 6. Jane Lyimo **– MKURABITA**	7. Bi. Anzanukye Mselela - **TASAF** 8. Bw. Ombeni Sereri - **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo** 9. Bw. Ahmed Salmin - **UTT AMIS** 10. Bi. Happy Mwaipopo - **Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara** 11. Bw. Godfrey Mwatiza - **Wizara ya Feda na Mipango** 12. Bi. Nyakaho Mahemba **- NEEC**

Majukumu ya Kamati zote za Maandalizi yalikuwa kama ifuatavyo:

i. Kuchagua viongozi kwa kila Kamati;
ii. Kuandaa mpango kazi wa maandalizi wa Maonesho ulio na mgawanyo wa majukumu na muda wa utekelezaji;
iii. Kupitia rasimu ya bajeti na kutoa maoni;
iv. Kutafuta pesa kwa ajili ya kufadhili shughuli za maonesho;
v. Kukaa vikao vya mara kwa mara kutathmini maandalizi ya maonesho na kutoa taarifa Baraza la Uwezeshaji;
vi. Kutoa ushauri kwa Baraza kuhusu namna bora ya kufanikisha maonesho;
vii. Kutoa taarifa ya orodha ya taasisi ambazo zitakazoombwa mchango Baraza la Uwezeshaji ili kuepusha migongano ya maombi ya fedha kwa taasisi moja; na
viii. Kutafuta watoa huduma wa shughuli za maonesho.

4.0 MAONESHO YA TANO (5) YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Maonesho ya tano (5) ya mifuko yalifanyika katika kanda ya mashariki tarehe 08 -14 Mei, 2022 katika viwanja vya Jamhuri Mkoani Morogoro. Mikoa iliyohusika katika kanda hiyo ni Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Lindi na Mtwara. Maonesho haya yalikuwa na madhumuni yafuatayo: -

i. Kukuza uelewa wa wananchi kuhusu uwepo, majukumu na vigezo vinavyotumika katika kutoa huduma za mifuko na program za uwezeshaji na hivyo kuwahamasisha wananchi ili waweze kunufaika na fursa zilizopo katika mifuko hiyo;

ii. Kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza katika miradi yenye kuleta faida;

iii. Kuhamasisha kuanzishwa na kuimarishwa kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kwa ajili ya kujiwekea akiba na kukopeshana ili kupata mitaji ya kuwekeza katika miradi ya kiuchumi;

iv. Kuwaunganisha wajasiriamali na masoko;

v. Kuwakutanisha wajasiriamali na watoa huduma mbalimbali wa Serikali na binafsi watakaosaidia kuongeza thamani na kukuza biashara zao;

vi. Kutengeneza mtandao wa wajasiriamali na wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu; na

vii. Kuibua fursa za uwekezaji katika Mikoa ya Kanda

4.1 WASHIRIKI WA MAONESHO

Maonesho haya yyalihudhuriwa na wadau kutoka makundi mbalimbali kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini na orodha yake kuambatishwa nyuma ya taarifa hii:-

NA	KUNDI LA WASHIRIKI	IDADI YA TAASISI
1	Mifuko na Programu za Uwezeshaji	28
2	Wizara za Serikali Kuu	3
3	Taasisi za Serikali	19
4	Vyuo vya Elimu ya Juu	2
5	Sekta ya Fedha	9
6	Mikoa	4
7	Halmashauri	15
8	Sekta Binafsi	6
9	Wajasiriamali	243

4.1.1 WAJASIRIAMALI

Jumla ya wajasiriamali 243 kutoka katika mikoa minne (4) walifanikiwa kushiriki maonesho haya, aidha wajasiriamali hao walikuwa wakionesha bidhaa zinazohususha sekta mbalimbali kama vile Usindikaji wa Vyakula na kuongeza thamani ya mazao (Vileo, mchele, Asali,Mafuta ya alizeti, Viungo), mazao ya kilimo cha Mbogamboga, Ufugaji wa samaki na kuku, utengenaziji wa batiki na ushonaji wa nguo kwa jinsia zote na rika mbalimbali, Utengezaji wa majiko na mashine mbalimbali za uzalishaji mali, ngozi, vifaa vya Ujenzi, Ufumaji wa madhuria, sabuni za maji na miche, ushonaji wa vikapu na mabegi na ususi ya nyungo, uungaji vyuma, dawa za asili, taulo za kike, useketaji wa vikoi, blanketi na vitambaa vya kutandika katika masofa, Bidhaa za asili (*Culture*)-*African Crafts*, Miche ya matunda mbalimbali, ubunifu wa mashine za uzalishaji, vifaa tiba vya hospitali, na pembejeo za kilimo.

4.1.2 USHIRIKI WA WAJASIRIAMALI KIMKOA

Katika maonesho hayo, ushiriki wa wajasiriamali kimkoa ulikuwa kama ifuatavyo;

NA	MKOA	IDADI YA WAJASIRIAMALI	ASILIMIA (%)
1	Morogoro	164	67
2	Pwani	17	7
3	Dar es salaam	48	20
4	Shinyanga	14	6
JUMLA		**243**	**100**

4.1.3 USHIRIKI WA WAJASIRIAMALI KISEKTA

Kati ya wajasiriamali 243 walioshiriki kuonesha bidhaa zao kisekta, idadi kubwa ya wajasiriamali walishiriki kuonesha bidhaa zilizozalishwa/kutengeezwa kutoka sekta ya Usindikaji wa Vyakula na kuongeza thamani ya mazao (Vileo, mchele, Asali, Mafuta ya alizeti, Viungo), utengenaziji wa batiki na ushonaji wa nguo wa jinsia zote na rika mbalimbali na bidhaa za asili/utamaduni. Aidha, idadi ndogo ya wajasiriamali walitoka katika sekta ya utengenezaji wa vifaa vya ujenzi, vifaa tiba na uungaji wa vyuma kama mchanganuo unavyojuonesha katika jedwali hapa chini: -

NA	SHUGHULI ZA WAJASIRIAMALI WALIOSHIRIKI	IDADI YA WAJASIRIAMALI
1	Usindikaji wa Vyakula na kuongeza thamani ya mazao (Vileo, mchele, Asali, Mafuta ya alizeti, Viungo)	37
2	kilimo cha Mbogamboga	19
3	Ufugaji wa samaki na Kuku	6
4	Utengenaziji wa batiki na ushonaji wa nguo wa jinsia zote na rika mbalimbali	30

5	Utengezaji wa majiko na mashine mbalimbali za uzalishaji mali	5
6	Bidhaa za ngozi	15
7	Vifaa vya Ujenzi	2
8	Ufumaji wa madhuria	8
9	Sabuni za maji na miche	14
10	Ushonaji wa vikapu na mabegi na ususi ya nyungo	10
11	Uungaji vyuma	3
12	dawa za asili	19
13	Taulo za kike	8
14	Useketaji wa vikoi, blanketi	14
15	Bidhaa za asili (Culture)-African Crafts	21
16	Uuzaji wa Miche	4
17	Ubunifu wa mashine mbalimbali	13
18	Vifaa tiba	2
19	Pembejeo za Kilimo	13
	Jumla	**243**

5.0 MATUKIO YALIYOJIRI KATIKA KIPINDI CHA MAONESHO

Kulikuwa na matukio mbalimbali katika katika kipindi cha maonesho kama ifuatavyo: -

i. Hafla ya ufuanguaji wa Maonesho

ii. Matembezi ya wageni katika kipindi cha katikati cha maonesho

iii. Elimu ya madarasa kwa wajasiriamali

iv. Hafla ya utoaji wa tuzo, mikopo & ruzuku na ufungwaji wa maonesho

5.1 HAFLA YA UFUANGUAJI WA MAONESHO

Maonesho yalifunguliwa rasmi tarehe 09 Mei, 2022 saa 04:00 asubuhi na Waziri wa uwekezaji, Viwanda na Biashara aliyewakilishwa na Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Mhe. Martine Shigela, aidha wageni wengine waliohudhuria katika hafla hii ni pamoja na Mdhamini Mkuu wa Maonesho aambaye ni Mkuu wa Taasisi ya Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania (TACT), Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Morogoro, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro pamoja na Wakuu wa Taasisi mbalimbali kutoka katika sekta binafsi na za Serikali. Maelezo/maudhui ya hotuba za viongozi katika siku hiyo yalikuwa kama ifuatavyo: -

5.1.1 KATIBU MTENDAJI – NEEC

5.1.1.1 Alizungumzia historia na chimbuko la maonesho kwa kusema Maonesho ya kwanza yalifanyika mwaka 2017 (Dodoma); ya pili mwaka 2018 (Mbeya), ya tatu yalifanyika mwaka 2018 (Simiyu) na ya nne yalifanyika mwaka 2021 (Arusha);

5.1.1.2 Madhumuni ya maonesho ni kuonesha jitihada ambazo Serikali imeanzisha kutatua changamoto ya mtaji kwa wananchi;

5.1.1.3 Mafanikio yaliyopatikana kupitia utendaji wa Mifuko toka ianzishwe ni utolewaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi Trilioni 5.35 kwa wananchi zaidi ya elfu nane na kutengeneza ajira zaidi ya milioni 13; na

5.1.1.4 Alitaja matokeo tarajiwa kwa wananchi na Serikali baada ya maonesho haya ni pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi walio wengi kuhusu uwepo kwa mifuko hiyo na jinsi ya kunufaika nayo; kuongezeka kwa utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwekeza katika miradi ya kiuchumi yenye kuleta faida; Kuongezeka kwa urasimishaji wa biashara na ardhi kwa wananchi, Kuongezeka kwa mapato katika vyanzo mbalimbali vya Serikali Kuu, Kuongezeka na kuimarika kwa shughuli za uchumi katika sekta mbalimbali na pia hamasa kwa wananchi kutafuta vigezo vya kukopesheka, ikiwa ni pamoja na kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi kama SACCOS, VICOBA, n.k

5.1.2 MDHAMINI MKUU WA MAONESHO

Mdhamuni Mkuu alitoa maelezo kama ifuatavyo: -

5.1.2.1 Mfuko wa TACT unahudumia kundi kubwa la wakulima ambao hawakopesheki katika taasisi mbalimbali za fedha;

5.1.2.2 Mfuko unatoa mikopo ya kuanzia $200,000(TZS MILIONI 500) wa kundi moja la wakulima;

5.1.2.3 Ameishauri Serikali kutunga Sera ya *LAND FOR EQUITY* ambayo ndio changamoto kubwa ya wakulima wadogo wanapotaka kufanya kazi ya kilimo kwa kushirikiana na wawekezaji hasa wanaotoka nje ya nchi; na

5.1.2.4 Mfuko wa TACT Unafanya kazi moja kwa moja na mkulima mkubwa mwenye mkataba wa masoko, hivyo, mkulima huyu anawezeshwa ili aweze kuwasaidia wakulima wakulima wadogo.

5.1.3 MHE. MKUU WA WILAYA YA MOROGORO

Aliishauri Serikali kuhakikisha kuwa, inatumia mapato ya ndani ya Halmashauri (asilimia kumi) kuwekeza katika Mfuko wa TACT ili kuwasaidia wakulima wadogo, Hii ni baada ya kuonekana kuwa, mikopo inayotolewa kupitia mapato haya hairejeshwi na haina matokeo chanya baada ya wananchi kuwezeshwa

5.1.4 MHESHIMIWA MGENI RASMI

Hotuba ya Mgeni Rasmi ilikuwa na maelekezo yafuatayo: -

5.1.4.1 Alitoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya wa Mkoa wa Morogoro, Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Morogoro na watendaji waliochini yao watenge muda kuhudhuria maonesho;

5.1.4.2 Aliwaasa wanananchi wa Mkoa wa morogoro na Mikoa ya Kanda kuhakikisha kuwa, wanahudhuria maonesho haya ili kujua fursa na kuzichangamkia fursa;

5.1.4.3 Aliigiza mifuko na Programu za uwezeshaji kujikita katika utoaji wa elimu kwa wananchi kabla ya kutoa mikopo;

5.1.4.4 Aliagiza Mifuko ifikishe huduma kwa wakulima wadogo ambao ndio kundi kubwa katika nchi ya Tanzania;

5.1.4.5 Aliaagiza Taasisi ya NSSF ifikishie huduma zao kwa wakulima wadogo wadogo kama inavyofanya katika sekta nyingine;

5.1.4.6 Aliiagiza Mifuko iendelee kufungua matawi katika sehemu za nje ya mji ambapo ndiko kundi kubwa la walengwa liliko; na

5.1.4.7 Baraza kufuatilia utungwaji wa Sera ya '***Land for equity'*** itakayowasaidia wakulima wadogo kwa kuwaunganisha na wawekezaji.

5.2 MATEMBEZI YA WAGENI KATIKA KIPINDI CHA SIKU ZA KATIKATI KATIKA WIKI YA MAONESHO

Maonesho haya yalihudhuriwa na wageni mbalimbali katika siku za katikati waliokuja kujionea fursa mbalimbali zinazotolewa na Mifuko ya Uwezeshaji ili waweze kuzifikisha kwa wadau wao, aidha wageni hawa walitoa pangiwa ratiba na kuwekewa utaratibu wa kutembelea washiriki wa maonesho, wageni walitembelea maonesho haya katika siku za katikati walikuwa ni: -

5.2.1 Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Zainab R. Telack;

5.2.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Bora;

5.2.3 Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Morogoro;

5.2.4 Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro;

5.2.5 Wakurugenzi wa Halmashauri toka Mkoa wa Morogoro;

5.2.6 Mkuu wa Wilaya ya Gairo;

5.2.7 Mkuu wa Wilaya ya Morogo Mjini;

5.2.8 Mkuu wa Wilaya ya Ulanga; na

5.2.9 Mkuu wa Wilaya ya Malinyi.

5.3 VIPINDI VYA UTOAJI WA ELIMU KWA WAJASIRIAMALI

Baraza kwa kutambua umuhimu wa kazi za wajasiriamali iliamua kutenga sehemu maalum ya darasa lililokuwa likitoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wajasiriamali. Mafunzo hayo yamesaidia wajasiriamali kujitambua na kupanua uelewa wao katika masuala muhimu katika kukuza na kurasimisha biashara zao.

Jumla ya Wajasiriamali 283 na waratibu wa madawati ya uwezeshaji 38 walinufaika na mafunzo hayo kupitia mada 15 zilizowasilishwa. Mada zilizowasilishwa na wawasilishaji wake ni kama inavyoonekana katika **Jedwali hapa chini**

NA	**MADA**	**MWASILISHAJI**
1	Dhana ya Ujasiriamali (Sifa ya Mjasiriamali na Elimu ya Kujitambua)	SIDO MOROGORO
2	Viwango na Ubora wa bidhaa	TBS
3	Ujasiriamali na Masoko	TACT
4	Usajiliwajina la biashara na faidazake	BRELA
5	Umuhimu wa Kujiunga katika Vikundi vya Kifedha	VICOBA FETA
6	Fursa za Mifuko na Programu za Uwezeshaji	NEEC
7	Fursa za Bima katika Vikundi na Mikopo	SANLAM General Insurance/CMSA
8	Fursa za Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Vya Kati (SANV Viwanda Scheme)	SIDO MOROGORO
9	Fursa za Bima ya mazao na vikundi	NIC Tanzania Ltd/CMSA
10	Aina za leseni za Biashara na Faida zake	AfisaBiashara-Morogoro
11	Namna ya Kutengeneza Batiki	Moro Batiki

12	Fursa za Uwekezaji	UTT AMIS
13	Usindikaji wa Vyakula	SIDO Morogoro
14	Urasimishaji wa Ardhi na Biashara	MKURABITA
15	Uratibu wa uanzishwaji na Uendelezaji wa Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	NEEC

5.4 HAFLA YA UTOAJI WA TUZO NA UFUNGWAJI WA MAONESHO

Maonesho haya yalihusisha utoaji wa tuzo kwa lengo la kutoa pongezi kwa juhudi zilizofanywa washiriki ili kuongeza hamasa na ushindani na kuwapa moyo ili waendelee kutoa huduma kwa wananchi. Kamati maalum isiyofungamana upande wowote iliundwa maalum ili kuifanya kazi hii,

Kulikuwa na makundi sita yaliyoshindanishwa na kila kundi lilitoa mshindi wa wa kwanza hadi wakwanza hadi watatu. Aidha, kila mshindi alipewa ngao na cheti cha ushindi. Washindi kwa kila kundi waliokabidhiwa tuzo zao na Mheshimiwa Mgeni Rasmi walikuwa kama ifuatavyo: -

5.4.1 KUNDI LA SEKTA YA FEDHA

Mshindi wa Tatu: CMSA
Mshindi wa Pili: Vision Fund Tanzania
Mshindi wa Kwanza: Benki ya Equity

5.4.2 KUNDI LA HALMASHAURI

Mshindi wa Tatu: Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro
Mshindi wa Pili: Manispaa ya Morogoro
Mshindi wa Kwanza: Jiji la Dar Es Salaam

5.4.3 KUNDI LA TAASISI ZA KISERIKALI

Mshindi wa Tatu: NSSF
Mshindi wa Pili: Brela
Mshindi wa kwanza: Shirika la Posta Tanzania

5.4.4 KUNDI LA MIFUKO NA PROGRAM ZA UWEZESHAJI

Mshindi wa Tatu: TASAF
Mshindi wa Pili: BOT
Mshindi wa kwanza: PASS Trust

5.4.5 KUNDI LA WAJASIRIAMALI

Mshindi wa Tatu: Mrutu
Mshindi wa Pili: Kongano la Usindikaji wa Vyakula Mkoani Morogoro
Mshindi wa kwanza: Umoja wa Wajasiriamali wa mkoa wa Shinyanga

5.4.6 VYUO VYA ELIMU YA JUU

Mshindi wa Pili: Chuo vha Ardhi-Morogoro (ARIMO)
Mshindi wa kwanza: Chuo cha Sokoine Cha Kilimo (SUA)

5.4.7 WADHAMINI

Mshindi wa Tatu: e-GA
Mshindi wa Pili: TTCL
Mshindi wa kwanza: Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania (TACT)

5.5 HAFLA YA KILELE CHA MAONESHO

Maonesho yalifungwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyewakilishwa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Ashatu Kijaji, Aidha, kabla Mgeni Rasmi hajachukua nafasi yake, viongozi mbalimbali walipata nafasi ya kutoa hotuba zao kama ifuatavyo; -

5.5.1 MAELEZO YA HOTUBA YA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Katibu Mtendaji alizungumzia mafanikio ya utendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji pamoja na kuainisha changamoto ambazo Baraza inakumbana nazo kiutendaji, maelezo ya hotuba yake yalikuwa kama ifuatavyo: -

5.5.1.1 Mifuko ya uwezeshaji hadi Desemba, 2021 imefanikiwa kutoa mikopo na dhamana zenye thamani ya shilingi Trilioni 5.38 kwa wajasiriamali 8,829,595 wakiwemo wanawake 4,596,602 na wanaume 4,232,993;

5.5.1.2 TASAF imefanya uhawilishaji wa ruzuku yenye thamani ya shilingi 1,196,268,601,843 kwa kaya maskini na kuwanufaisha wananchi 4,843,329 wakiwemo wanaume 2,146,867 na wanawake 2,696,462;

5.5.1.3 Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati *(SANVN Viwanda Scheme)* umetoa yenye jumla ya thamani ya Shilingi 1,746,557,651 kwa miradi 32 katika mikoa 8.

5.5.1.4 Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi 991 yakiwemo majukwaa 23 katika ngazi ya mkoa, 144 katika ngazi ya Halmashauri za wilaya, 302 katika ngazi ya kata na majukwaa 522 katika ngazi ya kijiji yameanzishwa;

5.5.1.5 Kuanzishwa kwa vituo vya uwezeshaji kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2020 Ibara ya 26 (K). Nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma za kuwawezesha wananchi kiuchumi zinapelekwa karibu na wananchi. Huduma hizi ni pamoja na: mikopo, mafunzo, urasimishaji wa biashara, ujuzi wa wafanyabiashara, uongezaji thamani ya mazao, elimu ya kodi na upatikanaji wa masoko. Hadi Desemba, 2021 jumla ya vituo vya uwezeshaji 17 vimeanzishwa katika mikoa 6 ya Shinyanga (Kahama), Geita, Singida, Rukwa (Sumbawanga), Kigoma (Vituo 6) na Dodoma (Vituo 7);

5.5.1.6 Changamoto zilizowasilishwa na katibu Mtendaji kwa upande wa Mifuko ya uwezeshaji ni kama ifuatavyo: -

5.5.1.6.1 Kiwango kidogo cha upatikanaji wa huduma za fedha katika maeneo ya pembezoni na vijijini. Hali hii inakwamisha wafanyabiashara waliowekeza maeneo ya pembezoni na vijijini kushindwa kupanua biashara na wananchi kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

5.5.1.6.2 Ukosefu wa mitaji kwa wananchi wanaohitaji kuanzisha au kukuza biashara kutokana na ukosefu wa dhamana.

5.5.1.6.3 Gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma za fedha kutokana na riba kubwa na kufanya gharama kubwa za upatikanaji wa mikopo.

5.5.1.6.4 Kutorejeshwa kwa mikopo hasa inayotolewa na Mfuko wa Kuwawezesha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri.

5.5.1.6.5 Ukosefu wa dhamana kwa wananchi wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati kutokana na eneo kubwa la ardhi nchini kutopimwa au kurasimishwa. Ardhi ni chombo cha uwezeshaji kwa kutumika kama dhamana ya mikopo.

5.5.1.6.6 Uwepo wa kaya maskini zisizo na sifa za umaskini kuingizwa katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa TASAF kwa sababu ya baadhi ya wanajamii kutokuwa wawazi na kusema ukweli kwenye mikutano mikuu maalum iliyopitisha majina ya kaya maskini.

5.5.2 MAELEKEZO YA HOTUBA YA MGENI RASMI

5.5.2.1 Mikoa yote pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ijenge vituo vya uwezeshaji ili kusongeza huduma kwa wananchi kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020;

5.5.2.2 Taasisi za Serikali pamoja na za sekta binafsi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji, benki na taasisi za fedha ziwasilishe taarifa za wakopaji katika Taasisi za Kuchakata Taarifa za Mikopo (*Credit* Reference *Bureau*) ili kuhakiki taarifa za wakopaji kwa lengo la kuwa na takwimu sahihi za wakopaji na kumbukumbu zao za urejeshaji;

5.5.2.3 Ofisi ya Rais - TAMISEMI itengeneze mfumo wa kielektroniki ambao utawezesha kuhakiki taarifa za madeni ya wanufaika ili kuondoa sintofahamu inayojitokeza mara kwa mara. Pia nawaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakiki taarifa za madeni ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwezesha mikopo hii itolewe kwa walengwa waliokusudiwa pamoja na kuimarisha usimamizi wa Mfuko huu;

5.5.2.4 Mikoa yote itenge na kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo;

5.5.2.5 Mawaziri wa Nishati; Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na Ujenzi na Uchukuzi kupitia REA, UCSAF, TANROADS na TARURA wapeleke huduma zao hasa maeneo ya pembezoni miji ili kuongeza huduma na kuchochea shughuli za kiuchumi;

5.5.2.6 Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi aongeze kasi ya upimaji wa ardhi na urasimishaji wa maeneo ikiwemo viwanja na mashamba ili kuwawezesha wananchi wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati kutumia ardhi kama chomo cha uwezeshaji kwa lengo la kupata hati ambazo zinahitajika kama dhamana.

5.5.2.7 TASAF na Mikoa yote iimarishea mfumo wa usimamizi ili kuhakikisha wanufaika wa TASAF wanafuzu kwa lengo la kuweza kujitegemea kwa wale wenye nguvu ya kufanya shughuli za kiuchumi na kupunguza mzunguko wa umaskini katika kaya na Taifa kwa ujumla; na

5.5.2.8 Wizara na taasisi za Serikali na sekta binafsi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji zinazotoa mikopo na dhamana ya mikopo pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke na kutekeleza mikakati ya uhakika itakayochochea wakopaji kurejesha mikopo kwa hiari ili kusaidia ukuaji na uendelevu wa mifuko na programu za uwezeshaji.

5.5.3 UTOAJI WA MIKOPO NA MIKATABA YA RUZUKU

Mheshimiwa mgeni rasmi alifanikiwa kukabidhi mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 970 kwa wajasiriamali 6 na ruzuku zenye thamani ya shilingi milioni 365 kwa taasisi 63 zinazojihusisha na utunzaji wa misitu na mazingira. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia taasisi ya PASS Trust, EFTA Tanzania na SELF Microfinance na ruzuku ilitolewa kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania.

Aidha, mikopo hiyo ilijumuisha utoaji wa vifaa vya mbejeo za kilimo ambavyo ni Trekta mbili na ***Combined Harvester*** 2,

6.0 TAAARIFA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kamati ya maandalizi ya maonesho ilifanya tathmini ya maonesho kwa kugawa fomu kwa washiriki ili kupata mrejesho ambao utaliwezesha Baraza kujifunza na kuboresha maonesho kwa miaka ijayo. Changamoto zilizowasilishwa na washiriki pamoja na maoni/mapendekezo yao ni kama ifuatavyo: -

6.1 CHANGAMOTO ZILIZOBAINISHWA NA WASHIRIKI

6.1.1 Mahudhuruo hafifu ya wananchi yaliyotokana na mpango mbovu wa matangazo;

6.1.2 Huduma za kijamii zisizoridhisha kama vile huduma za vyoo ndani ya uwanja kutototesheleza mahitaji, kutokuwa na huduma ya chakula;

6.1.3 Viwanja vya maonesho kuwa nje ya mji hivyo kuathiri mahudhurio ya wananchi;

6.1.4 Gharama za ushiriki za maonesho kwa taasisi kuwa juu ukilinganisha na maonesho mengine

6.1.5 Mabanda ya wajasiriamali kuwa nyuma, hivyo wananchi wanaotembelea maonesho kutofahamu maeneo walipo;

6.1.6 Kutokuwa na nafasi, njia au barabara katikati ya mabanda kulikopelekea kutokuwa na mawasiliano kati ya mabanda ya taasisi na mabanda ya wajasiriamali;

6.1.7 Kutokuwa na Sare ya ushiriki;

6.1.8 Wageni rasmi kuishia kutembelea mabanda ya Taasisi hivyo mabanda ya wajasiriamali kutotembelewa;

6.1.9 Kutotolewa mapema kwa ratiba za kila siku hivyo inawawiza vigumu washiriki kujiandaa

6.1.10 Idadi ndogo ya wafanya usafi na kupelekea mazingira ya viwanja kama vyoo kuwa machafu;

6.1.11 Muziki kuwa juu hivyo kufanya usikivu kuwa mdogo kwa wateja;

6.1.12 Kutokuwa na uhalisia wa ratiba za kila siku;

6.1.13 Magari ya matangazo yalionekana kupita katika mida ya mchana badala ya jioni na usiku ambapo watu wanakuwa wametulia majumbani;

6.1.14 Ratiba ya kufungua na kufunga kutokuwa wazi kwa washiriki;

6.1.15 Katazo la taasisi kuweka mabango yao katika viwanja vya maonesho

6.1.16 Gharama kubwa za ushiriki wa maonesho zisizoendana na huduma ambazo NEEC imetoa; na

6.1.17 Madarasa ya uelemishaji kufanyika mida ya mchana tu na muda unaotolewa kwa wawasilishaji wa mada kuwa mchache.

6.2 MAPENDEKEZO KWA MAONESHO YAJAYO

6.2.1 Bajeti ya matangazo iongezwe ili kuhakikisha kuwa uwepo wa maonesho unajulikana na watu wengi;

6.2.2 Matangazo ya maonesho yafanyike miezi miwili (2) kabla na uhamasishaji uanzie kuanzia ngazi ya kata;

6.2.3 Maonesho yajayo yafanyike katika viwanja vilivyokatikati ya mji na ikiwezekana viwanja hivyo viwe katika eneo lililo wazi, rafiki na lenye kuhamasisha wananchi kuhudhuria;

6.2.4 Gharama za maonesho zipungue ili kuendana na hali halisi za fedha za wadau;

6.2.5 Baadhi ya mabanda ya wajasiriamali yakae mbele pamoja na mifuko ya uwezeshaji;

6.2.6 Bajeti ya sare kwa washiriki iwekwe au iongezwe katika mchango wa ushiriki;

6.2.7 Maonesho yafanyike katika tarehe za mwisho wa mwezi na sio katika kati ya mwezi kama ilivyofanyika kwa maonesho haya;

6.2.8 Ratiba za kila siku ziwe zinatolewa siku moja kabla kama ilivyo kwa maonesho mengine, hii inawasaidia washiriki kuweza kujiandaa na kuwataarifu wakuu wa zao;

6.2.9 Kuwe na kamati maalumu inayosimamia usafi wa mazingira hasa vyooni;

6.2.10 Ratiba za kila siku zithibitishwe kabla ya kutolewa

6.2.11 Magari ya matangazo yawe yanatangaza mida ya jioni na usiku badala ya mchana tu;

6.2.12 Ratiba ya kufungua na kufunga zinapaswa ziandaliwe mapema na kutumwa kwa wadau siku moja kabla ili waweze kuziwasilisha kwa wakuu wao wa kazi;

6.2.13 Uratibu wa wageni waalikwa kupita katika mabanda uimarishwe uimarishwe na uhakikishe kuwa washiriki wote wanatembelewa;

6.2.14 Mpangilio wa uwekaji wa mabana ya matangazo katika viwanja vya maonesho na barabarani upitiwe na kuimarishwa na kuruhusu wadau wanaotaka kuweka matangazo wafanye hivyo; na

6.2.15 Gharama za maonesho zipitiwe ili ziendane na huduma zinazotolewa ili zifanane na maonesho yanayoandaliwa na taasisi nyingine.

Kiambatisho Na. 1: Taasisi zilizoshiriki Maonesho kimakundi

BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

TAASISI ZILIZOSHIRIKI KATIKA MAONESHO YA TANO (5) YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

1.0 MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

1.1 Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania (TACT)
1.2 PASS Trust
1.3 Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Mauzo ya Bidhaa nchi za Nje
1.4 Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasirimali Wadogo na wa Kati wa BOT (SIDO-SMEs)
1.5 Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Wananchi wenye kipato cha chini
1.6 Mfuko wa Kuendeleza Wajasirimali Wananchi (NEDF)
1.7 Mfuko wa Dhamana kwa Wajasirimali Wadogo na wa Kati wa SIDO(SIDO-SMEs)
1.8 Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa wakulima Wadogo (SGCS)
1.9 African Guarantee Fund (AGF)
1.10 Mfuko wa Mzunguko wa Mkoa (SIDO RRF)
1.11 Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Vya Kati (SANVN Viwanda Scheme)
1.12 UTT AMIS
1.13 Mfuko wa SELF Microfinance
1.14 Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara kwa Wanyonge
1.15 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF)
1.16 Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu
1.17 Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF)
1.18 EFTA Tanzania
1.19 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
1.20 Mfuko wa Misitu Tanzania
1.21 Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki
1.22 Mfuko wa Malikale
1.23 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori (TWPF)
1.24 Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF)
1.25 Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali
1.26 Mfuko wa Fidia wa Ardhi Tanzania
1.27 Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (MEF)
1.28 Mpango wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu

2.0 WIZARA ZA SERIKALI

- 2.1 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- 2.2 Wizara ya Fedha na Mipango
- 2.3 Wizara ya Maji

3.0 TAASISI ZA SERIKALI

- 2.1 Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)
- 2.2 NEEC
- 2.3 Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)
- 2.4 Wakala ya Usajili Biashara na Leseni (BRELA)
- 2.5 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)
- 2.6 PURA
- 2.7 Shirika la Hifadhi za Jamii (NSSF)
- 2.8 NHIF
- 2.9 TBS
- 2.10 TAWA
- 2.11 TFS
- 2.12 SHIRIKA LA POSTA TANZANIA
- 2.13 TMDA
- 2.14 EPZA
- 2.15 FCC
- 2.16 Bodi ya Koroshi Tanzania (CBT)
- 2.17 NBS
- 2.18 TANROADS
- 2.19 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

4.0 VYUO VYA ELIMU YA JUU

- 3.1 Chuo Cha Kilimo Cha Sokoine (SUA)
- 3.2 Chuo Cha Ardhi Morogoro (ARIMO)

5.0 SEKTA YA FEDHA

- 4.1 SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA (NICT)
- 4.2 SANLAM GENERAL INSURANCE
- 4.3 TIRA
- 4.4 SANLAM LIFE ASSURANCE
- 4.5 NMB BANK T. LTD
- 4.6 EQUITY BANK
- 4.7 VISIONMICROFINANCE FUND
- 4.8 PBZA
- 4.9 TCB Commercial Bank

6.0 MIKOA NA HALMASHAURI

6.1 MKOA WA MOROGORO NA HALMASHAURI ZAKE

6.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro
6.1.2 Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba
6.1.3 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa
6.1.4 Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara
6.1.5 Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
6.1.6 Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi
6.1.7 Manispaa ya Morogoro
6.1.8 Halmashauri ya Wilaya ya Gairo

6.2 MKOA WA DAR ES SALAAM NA HALMASHAURI ZAKE

6.2.1 Manispaa ya Ilala
6.2.2 Manispaa ya Ubungo
6.2.3 Manispaa ya Temeke
6.2.4 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

6.3 MKOA WA SHINYANGA

6.3.1 Manispaa ya Kahama

6.4 MKOA WA PWANI

6.4.1 Halmashauri ya Mji wa Kibaha

7.0 SEKTA BINAFSI

7.1 TCCIA
7.2 GSI TANZANIA
7.3 TWCC
7.4 Majukwaa ya Wanawake yaUwezeshaji Wananch Kiuchumi (Mkoa waShinyanga na Morogoro)
7.5 Moro Batiki
7.6 SUGEKO

8.0 WAJASIRIAMALI

WAJASIRIAMALI – 243